Jina _____ Nambari _____

Sahihi ya mtahiniwa _____

Tarehe _____

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**INSHA**
**JULAI / AGOSTI 2011**
**MUDA : 1 ¾**

**TATHMINI YA PAMOJA YA WILAYA YA MAKUENI / KATHONZWENI 2011 (MAKA)**
**Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**SAA : 1 ¾**

**MAAGIZO**

(a) Andika Insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima.
(b) Kisha chagua Insha moja nyingine kutoka hizo tatu zilizobakia.
(c ) Kila Insha isipungue maneno mia nne. (400)
(d) Kila Insha ina alama 20.

***Kijitabu hiki kina kina kurasa 2 ambazo zimepigwa chapa***

***Fungua ukurasa***

1. Wewe ni katibu wa kamati ya elimu wilayani. Andika kumbukumbu za mkutano uliojadili changamoto zinazokabili shule za upili wilayani.

2. Ajali za barabarani ni changamoto kubwa katika nchi yetu. Jadili.

3. Usipoziba ufa utajenga ukuta.

4. Andika Insha itakayomalizika kwa maneno haya.

   …… ni wakati huo alipopata mwanya wa kutoweka huku akimwacha kijana huyo akilia kwi kwi kwi akiwa kwenye mtaro wa maji taka.

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**INSHA**
**JULAI / AGOSTI 2011**

**TATHMINI YA PAMOJA YA WILAYA YA MAKUENI / KATHONZWENI 2011 (MAKA)**
**Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**

## MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

Swali la 1
1. Sura ya kumbukumbu sharti izingatiwe.
2. Kichwa kinachofaa mada, mahali, tarehe na wakati itajwe.
3. Mwanafunzi sharti azingatie sehemu ya changamoto na suluhisho / mapendekezo.

Changamoto
- Ukosefu wa waalimu.
- Ukosefu wa vifaa mf. Maabara.
- Uzembe miongoni mwa wanafunzi.
- Ongezo la wanafunzi.
- Madawa ya kulevya.
- Njaa.
- Ukosefu wa salama.
- Magonjwa.
- Uhaba wa fedha.
- Viwango duni vya elimu.
- Utamaduni.
- Ukosefu wa ajira – baada ya kuhitimu.
- Athari za kisiasa.
- Sera za elimu.
- Ongezeko la mayatima – Athari za ukimwi.
- Umaskini.

Suluhisho
- Serikali kuajili waalimu.
- Serikali na mashirika yasiyo ya serikali iingilie.
- Wanafunzi wapewe mawaidha mwafaka.
- Shule zijenge darasa zaidi.
- Ushauri kwa wanafunzi kuhusu madawa ya kulevya. Kuhusisha washika dau wengine katika jamii.
- Misaada ya chakula shuleni.
- Serikali iongeze maafisa wa usalama.
- Wanafunzi washauriwe kuhusu magonjwa kama vile ukimwi na magonjwa ya zinaa.
- Serikali ipigane na tamaduni zinazogandamiza sera za elimu mf. Ndoa za mapema / za lazima.

***Kijitabu hiki kina kurasa 4 ambazo zimepigwa chapa***

***Fungua ukurasa***

Swali la 2

Kinachosababisha

- Barabara mbovu .
- Madereva wasiohitimu.
- Madereva walevi.
- Mwendo wa kasi.
- Kutofuata sheria za barabarani.
- Magari mabovu mabovu.
- Kutowajibika kwa polisi wa trafiki.
- Kuzidisha uzani wa mizigo na abiria.
- Ukosefu wa vidhibiti mwendo n.k.

Suluhisho

- Vidhibiti mwendo.
- Hatua kuchukuliwa kwa wanaokiuka sheria za barabarani.
- Magari mabovu kutoruhusiwa barabarani.
- Askari wa trafiki wawajibike.
- Barabara zikarabatiwe n.k.

Swali la 3

Swali la methali

- Mwanafunzi atoe maana wazi na maana fiche
- Mwanafunzi atunge kisa au visa vitakavyoafiki maana ya methali hii.
- Sharti tuone mhusika asiyejali kurekebisha kasoro Fulani ambayo inakua na kuleta madhara makubwa.
- Madhara haya yanamletea hasara kubwa na anabaki kujuta.

Swali la 4

Swali la mdokezo.

- Mwanafunzi sharti akamilishe kwa maneno aliyopewa.
- Akiongeza au kupunguza maneno haya huwa amejitungia swali na anatuzwa bakhshishi Bk 01.
- Lazima atunge kisa au visa vitakavyoingiliana vizuri na maneno aliyopewa.
- Shart tuwaone wahusika wawili.
    (i) Kijana aliyekuwa akilia na kwa nini.
    (ii) Aliyetoroka – Kwa nini alitoroka.

Maagizo zaidi ya usahihishaji.

(i) Kosa la hijai liadhibiwe linapotokea kwa kupigia msitari _____.
(ii) Kosa la sarufi liadhibiwe linapotokea vistari ═══ .
(iii) Atakayekosa sura ya Insha aondolewe alama 4S
(iv) Atakayekosa kutimiza urefu aondolewe 2U
(v) Atakayeegemea upande mmoja aondolewe 4M
(vi) ∧ hutumiwa kuachwa kwa neno.
(vii) √ kuonyesha msamiati bora – juu ya neno hilo.
(viii) X Msamiati usiofaa – juu ya neno lenyewe.

JINSI YA KUTUZA ALAMA

1. Kiwango cha D (alama 01 – 05 )
Hutuzwa insha ambayo:-
(a) Haieleweki.
(b) Imeandikwa kwa lugha hafifu k.m Isiyojulikana kama ni Kiswahili au lugha nyingine.
(c ) Haijaonyesha uwezo wa kutumia lugha ya Kiswahili kwa njia inayofaa.
(d) Ina makosa ya kila aina km. Sarufi, mtindo, maelezo, hijai n.k.
(e) Mtindo mbovu – k.m Kuvuruga kanuni maalum za Insha Fulani.

2. Kiwango cha C (alama 06-10 )
Insha katika kiwango hiki huwa:-
(a) Mada haijakuzwa na kuendelezwa vizuri.
(b) Ujumbe haukuwasilishwa kwa njia inayovutia.
(c ) Kuna makosa mengi ya sarufi, msamiati, hijai n.k.
(d) Hakuna ubunifu wa kutosha.
(e) Sentensi zimeakifishwa vibaya.
(f) Hakuna msamiati wa kuvutia au mwafaka.

3. Kiwango cha B (11-15)
(a) Anaonyesha kuimudu lugha vilivyo.
(b) Mtahiniwa anaonyesha au anadhihirisha kwamba anaweza kutumia lugha kwa kueleza.
(c ) Miundo imetumiwa tofauti katika sentensi vizuri.
(d) Uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha umejitokeza vilivyo.
(e) Mada imekuzwa na kuendelezwa kikamilifu.

B- (11-12 )
(a) Ujumbe huwasilishwe kwa njia tofauti tofauti kutumia au kuonyesha hoja.
(b) Mtiririko mzuri wa mawazo umejitokeza.
(c ) Huwa kuna uwezo wa kutumia miundo tofauti tofauti ya sentensi ambayo mtahiniwa ameonyesha.
(d) Makosa ni machache ya hapa na pale.

B( Wastani ) 13
(a) Lugha nzuri imedhihirika na hali ya kuimudu kuonyeshwa.
(b) Ujumbe umewasilishwa waziwazi kwa mawazo yanayodhihirika.
(c ) Matumizi ya lugha yenye mnato yamejitokeza.
(d) Mifano mwafaka michache imetumiwa.
(e) Matumizi ya tamathali za usemi yamedhihirika.
(f) Makosa yanaweza kutokea ya hapa na pale lakini si mengi.

B+ (Juu) 14-15
(a) Mawazo ya mtahiniwa yamedhihirika.
(b) Mtahiniwa amewasilisha ujumbe kwa njia inayovutia na kwa urahisi.
(c ) Makosa ya hapa na pale yameonekana ambayo mtahiniwa hakudhamiria kufanya.
(d) Uteuzi wake wa msamiati ni mzuri.
(e) Sarufi yake ni nzuri na uakifishaji wake ni mzuri.

Kiwango cha A (16-20)
(a) Mwandishi anadhihirisha ujuzi wa lugha yenye mnato.
(b) Ubunifu wa mawazo yenye kudhihirika  na kuvutia umeonyeshwa kwa ustadi.
(c ) Uwezo unajitokeza kwa kutumia tamathali za lugha ili kutoa hisia zake kwa njia bora na urahisi.
(d) Uumbaji wake na Insha hudhihirisha ukakamavu wake kimawazo na mpangilio mzuri na hali ya kumvutia msomaji wake .
(e) Kazi nadhifu na hati nzuri, na huzingatia urefu unaotakikana.

A- (16-17)
(a) Ukakamavu wa mwandishi umedhihirishwa.
(b) Mtiririko umelingana na mada.
(c ) Lugha imepambwa kwa kutumia tamathali za usemi
(d) Matumizi mazuri ya msamiati na sarufi huwa yamezingatiwa.

Jina _____ Nambari _____

Sahihi ya mtahiniwa _____

Tarehe _____

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**LUGHA**
**JULAI / AGOSTI 2011**
**MUDA : 2 ½**

**TATHMINI YA PAMOJA YA WILAYA YA MAKUENI / KATHONZWENI 2011 (MAKA)**
**Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**SAA : 2 ½**

**MAAGIZO**

(a) Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Jibu maswali yote.
(c ) Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kitabu hiki cha maswali.
(d) Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote zimepiwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMAL | 80 | |

***Kijitabu hiki kina kina kurasa 10 ambazo zimepigwa chapa***

***Fungua ukurasa***

**1. UFAHAMU**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Miongoni mwa maonyesho ambayo hufanywa kila mwaka mjini Lamu katika mwambao wa Kenya ni tamasha za kitamaduni zinazojumuisha ngoma, michezo mbalimbali na maonyesho ya sanaa.

Wazee waliovalia kanzu maridadi nyeupe sambamba na utamaduni wao hubeba bakora na kuziwekelea mabegani na kucheza taratibu kwa kufuata mdundo wa ngoma na zumari. Miongoni mwa ngoma wazichezazo wazee ni goma la siu kutoka mji wa Siu, Goma la Barani kutoka jamii ya wabajuni, Twari la Ndia kutoka Pate na Goma la Uta kutoka Lamu.

Bila shaka, kila aina ya mapigo katika mojawapo ya ngoma hizi huwasilisha ujumbe Fulani katika maisha ya kawaida, ila katika sherehe hizi za kila mwaka jukumu lake huwa ni kutumbuiza na kuendeleza utamaduni. Vile vile, huwa ni thibitisho kuwa ngomezi imekuwa sehemu adhimu katika maisha ya watu wa Pwani tangu jadi.

Michezo mbalimbali huvutia umati mkubwa wakati wa tamasha hizi. Katika mwakaa wa 2006, mchezo uliotia fora zaidi ni mashindano ya punda. Pengine kwa kuwa wakenya wamezoea kutazama mashindano ya farasi na kusahau kuwa punda ni binamu yake. Licha ya hayo mnyama huyo ni kiumbe muhimu wa uchukuzi sio tu katika visiwa vya Lamu bali pia katika sehemu Kavu za Kenya kama vile Ukambani na Umasaini.

Pengine ni kwa sababu ya umuhimu wake huo ambapo Jamal Mohamed Mshiriki wa tamasha hizo alimpagaza punda wake jina 'Nyonda' naye akampenda kweli kwa kuibuka mshindi wa mashindano hayo yaliyohudhuriwa na wageni wengi mashuhuri.

Mbali na mbio za punda, mashindano ya majahazi katika bahari huwa ni kivutio kikubwa zaidi . Je, umewahi kufikiria kuwa majahazi yaweza kushindana kama yafanyavyo magari ya mashindano ya safari Rally ? Watu hushuhudia jinsi mabaharia wanavyoweza kumudu mashua na majahazi na hata mitumbwi katika bahari.

Wasanii wa aina aina nao huwa hawaachwi nyuma. Huweza kuonyesha ufundi wao mbalimbali kama vile kusuka majamvi na vikapu, kuamba ngoma, kufua vyuma na kuandaa mpishi ya aina aina ya Kiswahili. Wasanii hawa hutengewa mahali pao maalum ambapo watu hutembelea na kujionea ufundi wao na hata kupata maelezo zaidi wakitaka.

Sherehe huwa hazijakamilika bila kuwepo kwa makundi ya waimbaji wa nyimbo za taarabu na waigizaji, hata ikiwa wataalikwa kutoka bara.

Katika mwaka wa 2006, kulikuwa na shughuli ya ziada katika sherehe hizo ambapo ulifanyika ufunguzi rasmi wa maonyesho ya malenga mashuhuri na mchongaji (wa mbao) aliyesifika marehemu Mohamed Abubakar kijumwa katika makavazi ya Lamu.

Hata hivyo, ni huzuni nyingi kuwa wakenya wengi hawawezi kuhudhuria tamasha hizi kwa sababu ya hali mbaya ya barabara, Wageni, wenye uwezo wa kusafiri kwa ndege na watu wachache wapatao nafasi kwa mabasi ya kawaida ndio pekee wanaoneemeka.

<u>Maswali</u>

1. Ngomezi hutekeleza majukumu gani katika tamasha za kila mwaka zifanyikazo katika mji wa Lamu? ( alama 2 )

_____

_____

_____

_____

_____

2. Taja aina zozote za ngoma ambazo huchezwa katika tamasha hizi. ( alama 2 )

_____

_____

_____

_____

3. Unafikiri ni kwa nini mashindano ya punda huvutia zaidi katika tamasha hizi. ( alama 2 )

_____

_____

_____

_____

4. Mwandishi anadhamiria kupitisha ujumbe gani anaposema kuwa punda ni binamu ya farasi ? ( alama2 )

_____

_____

_____

_____

5. Kwa jumla kwa nini punda ni maarufu kwa uchukuzi katika sehemu kavu za Kenya ? ( alama 2 )

_____

_____

_____

_____

6. Je, maonyesho yafanyikayo katika tamasha za kitamaduni yanafaa ? Thibitisha jawabu lako. ( alama 3 )

_____

_____

_____

_____

_____

_____

7. Andika maneno mengine yenye maana sawa na :

(i) Bakora _____

(ii) Nyonda _____ ( alama 2 )

2. UFUPISHO

Muhula wa tatu wa kidato cha nne ulikuwa wakati mgumu. Wanafunzi wa kidato cha nne walijitahidi kubukua na kudurusu kwa chudi na idili. Walikabiliwa na mtihani wa kitaifa. Mtihani wa kuhitimisha kazi ya miaka minne. Wengi walikuwa na hamu na ghamu ya kumaliza masomo.

Nilikuwa na tamaa ya kufuzu na kuingia chuo kikuu mwakani. Hamna msichana yeyote ambaye alishajiunga na chuo kikuu kutoka kijiji cha Misombe. Wengi wao walikomea darasa la saba au nane. Kuna wachache waliosoma hadi kidato cha pili kisha wakayakatiza masomo. Sio wasichana peke yao hata wavulana pia hamna hata mmoja aliyewahi kujiunga na chuo kikuu. Mvulana wa karibu aliyewahi kujiunga na chuo kikuu alikuwa mwenyeji wa kijiji cha Anzama. Hiki kilikuwa kijiji cha akina Bethsheba. Huyu alijiunga na chuo kikuu zamani, nadhani nikiwa katika darasa la nne au tano; sikumbuki sawasawa. Hivi sasa alikuwa amerudi kusomea digrii ya pili. Alifahamika kama Cedric Mwambe.

Matokeo ya mtihani wa mwigo yalishatoka sasa. Nilikuwa mwanafunzi wa pili katika orodha ya wanafunzi kumi bora. Wa kwanza alikuwa Catherine Ouko msichana mfupi sana; labda ndiye aliyekuwa mfupi kuliko wote shule nzima. Alikuwa na akili shupavu na sote tulimwogopa. Waalimu walimsifu sana. Bethsheba alikuwa nambari ishirini na mbili. Yeye hakujali sana. Alishanieleza mara kadha wa kadha kuwa hakuwa na nia ya kuyaendeleza masomo yake. Hakuona sababu ya kuyaendeleza; miaka hiyo ilimtosha. Alidai kuwa waliotakiwa kusoma ni wanaume wala sio wanawake ambao wangeishia kuwa watunzaji wa nyumba tu. Mimi sikuamini hivyo asilani. Hayo yalikuwa mawazo yaliyopitwa na wakati na kwa kiasi kikubwa niliamini kuwa huko kutosoma kwa wanawake ndiko kulikochangia katika kuwafanya wabakie palepale; kuzungukia palepale kama pia.

Rose Mafali alikuwa miongoni mwa wanafunzi wa mwisho mwisho. Hakujali wala kubali. Lake lilikuwa moja tu; tumalize shule akaolewe. Alishikilia kuwa hamkuwa na maana ya kuyaendeleza masomo ambayo yasingemfalia kitu katika maisha yake ya ndoa. Wengi wetu tulishindwa kumwelewa. Mimi nilijitahidi kumshawishi aachane na mawazo ya aina hiyo lakini ilikuwa mjango, haikufaa kitu.

Nakumbuka kuna siku moja nilikuwa maktabani, siku ya Jumamosi. Wanafunzi wengi walishatoka shule kwenda mjini baada ya kupewa idhini na mwalimu mkuu. Mimi sikuona haja ya kwenda huko. Huu ulikuwa wakati mzuri wa kuyabukua matabu yangu. Nilielekea maktabani. Siku hiyo sikuketi katika sehemu niliyoizoea. Niliamua kuketi pengine kwa vile hamkuwa na wasichana wengi siku hiyo. Walikuwepo watu wawili watatu. Viti vingi vilikuwa wazi. Nilichagua sehemu Fulani iliyokuwa karibu na dirisha. Dirisha hilo lilielekeana na barabara kuu ya kuja shuleni. Niliviweka vitabu vyangu mezani. Niliweka kile kibweta cha hisabati karibu na vilipokuwa vile vitabu. Nilikivuta kiti changu karibu na ile meza. Macho yalishawishika kuangalia huko. Hamkuwa na yeyote isipokuwa mfanyikazi mmoja wa shule aliyeonekana hukoo …, upande wa chini karibu na kidaraja kilichotangulia maungano ya barabara ya shule na baraste kuu ya kwenda mji wa Machakos. Alikuwa ameshika mundu wa kufyeka nyasi.

Niliviangalia vitabu vyangu. Nilichukua kitabu cha fasihi ya Kiingereza.. Hii ilikuwa riwaya ya Ngugi wa Thiong'o ya 'The River Between.' Ilinijuza kuirudia riwaya hii. Upya kabla mtihani ambao ungeanza baada ya mwezi mmoja. Haikuwa riwaya kubwa sana ila nilihisi ukinaifu na ukimwa Fulani wa kuirudia hadithi ambayo nilikumbuka. Lakini sikuwa na budi; ilinibidi kujigagamiza kuisoma. Nilishazisoma sura kadha. Niliifungua ile riwaya na kusomasoma hadi nilipofikia kile kisa cha Muthoni ambaye alinivutia kwa ujasiri wake.

Maswali

(a) Bila kubadilisha ujumbe, fupisha aya mbili za mwanzo kwa maneno kati ya 60-65. ( alama 8 )
(2 za utiririko )

Matayarisho

Jibu

(b) Kwa kurejelea wahusika wawili, thibitisha kuwa jamii inayorejelewa na mwandishi haikujali elimu ya mtoto wa kike. (Tumia maneno yasiyozidi 40) (alama 4, 1 ya utiririko )

Matayarisho

Jibu

MATUMIZI YA LUGHA (alama 40 )

(a) (i) Andika neno moja ili kuonyesha silabi inayoundwa na konsonati pekee. ( alama 1 )

_____

_____

_____

(ii) Onyesha mzizi wa neno lililopewa kualika. ( alama 1 )
Kualika

_____

_____

(b) Tunga sentensi moja kuonyesha upatanisho wa kisarufi wa nomino changarawe. (alama2 )

_____

_____

_____

_____

(c ) Tambua viwakilishi katika sentensi uliyopewa, (alama 2 )

Aliyewasili _____

_____

_____

_____

(d) Andika sentensi katika nafsi ya tatu umoja. (alama 2 )

_____

_____

_____

_____

(e) Yakinisha sentensi uliyopewa. ( alama 2 )
Kama sisomi kitabu hiki vizuri sitafuzu.

_____

_____

_____

_____

(f) Tunga sentensi kuonyesha kundi nomino lenye kiwakilishi na kivumishi. ( alama 2 )

_____

_____

_____

(g) Andika sentensi upya ukitumia urejeshi ufaao. ( alama 2 )
Mgeni alifika na akaondoka.

_____

_____

_____

_____

(h Changanua sentensi uliyopewa kwa mtindo wa jedwali. (alama 4 )
Dalili za ukimwi zinaweza kujificha sana.

_____

_____

_____

_____

_____

_____

(i) Kwa kutumia mzizi wa kitenzi ulichopewa onyesha kauli ya kitendwa ya kitenzi hicho. ( alama 2 )
{ - l - }

_____

_____

_____

_____

(j) Akifisha kifungu hiki. (alama 3 )
tuliondoka nairobi mwendo wa saa tatu asubuhi kwa sababu hatukutaka kutatizika njiani ilibidi tule mapema wajua watu husema cha mtu ni alo nacho tumboni

_____

_____

_____

_____

_____

(k) Tambua aina za mofimu zilizopigiwa kistari. ( alama 2 )
<u>Alisita</u> alipofika kwao saa <u>sita</u>.

_____

_____

_____

_____

(l) Kanusha sentensi hii. (alama 2 )

Tumechukua nguo chache kuuza.

_____

_____

_____

_____

(m) Iandike upya sentensi uliyopewa kwa kufuata maagizo yaliyotolewa. ( alama 2)

Nimemleta paka ili aue panya wote wanaotusumbua hapa kwetu nyumbani. ( Anza na panya wote )

_____

_____

_____

_____

(n) Badilisha sentensi ifuatayo ili iwe katika hali ya kuamuru. (alama 2 )

Baba ingia ndani.

_____

_____

_____

(o) Eleza maana mbili za sentensi hii. (alama 2 )

Jane alifagia chakula chote.

_____

_____

_____

_____

_____

(p) Bainisha kirai na utaje ni cha aina gani. (alama 2 )

Alimpiga kwa uhodari.

_____

_____

_____

_____

(q) Badilisha sentensi ifuatayo katika usemi halisi. (alama 2 )

Mzazi alisema ya kwamba angerudi siku iliyofuata.

_____

_____

_____

_____

(r ) Sahihisha sentensi ifuatayo. ( alama 1 )

Nipe kitabu chenye nilikupea.

_____

_____

_____

_____

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10 )

"Nimechunguza kuwa umeingiliana na vijana wabaya lakini yaelekea si hivyo; Hata hivyo matokeo ya muhula yalikuwa duni zaidi."

(a) Sajili hii hupatikana wapi? Toa thibitisho kutoka kwenye kifungu. (alama 2 )

_____

_____

_____

_____

(b) Jadili sifa mbalimbali za lugha ya sajili uliyoitaja hapo juu. (alama 8 )

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**LUGHA**
**JULAI / AGOSTI 2011**

**TATHMINI YA PAMOJA YA WILAYA YA MAKUENI / KATHONZWENI 2011 (MAKA)**
**Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. UFAHAMU

1. - Hutumbuiza
   Huendeleza utamaduni ( alama 2 )

2. - Twari la Ndia
   - Goma la Siu
   - Goma la Uta
   - Goma la Barani ( 4 x ½ = 2 )

3. - Punda anajulikana kama mnyama wa uchukuzi.
   - Punda ni mkaidi, wengi hufikiri hawezi kufunzika mambo ila vile mbio. ( alama 2 )

4. - Punda aweza kufunzwa kama afunzwavyo farasi.
   - Punda afaa kuonewa fahari kama aonewavyo farasi. ( alama 2 )

5. Sehemu nyingi kavu hazina barabara nzuri zinazoweza kupitika kwa magari, punda hufaa kwa uchukuzi.
   - Punda ni mkakamavu. Anastahamili palipo na ukame. ( alama 2 )

6. Naam / ndio
   - Ni sehemu ya utamaduni.
   - Ni burudani.
   - Ni kitega uchumi – watalii waweza kujionea kwa ada Fulani ya kiingilio. ( alama 3 )

7. - Bakora – fimbo
   - Nyonda – mapenzi ( alama 2 )

2. UPUFISHO

(a) (i) Muhula wa tatu wa kidato cha nne ulikuwa wakati mgumu.
(ii) Watahiniwa walikabiliana na mtihani wa kitaifa.
(iii) Walitamani kuyamaliza masomo.
(iv) Nilitamani kujiunga na chuo kikuu.

***Kijitabu hiki kina kurasa 4 ambazo zimepigwa chapa***

***Fungua kurasa***

(v) Hamna msichana aliyejiunga na chuo kikuu kutoka Misombe.
(vi) Wengi walikomea darasa la nane na wachache kidato cha pili.
(vii) Hamna mvulana pia aliyejiunga na chuo kikuu.
(viii) Mmoja aliyewahi alitoka Anzama, kijiji cha akina Bethsheba.
(ix) Alijiunga zamani na amesomea digrii ya pili.
(x) Alifahamika kama Cedric mwambe.

( Hoja 8 x 1 = alama 8 )
( 2 za utiririko )

(b) - Bethsheba hakuwa na nia ya kuyaendeleza masomo yake.
- Alidai waliotakiwa kusoma ni wanaume sio wanawake walioishi kuwa watunzaji wa nyumba.
- Rose mafali alikuwa miongoni mwa wanafunzi wa mwisho.
- Hakujali, alitaka amalize shule aolewe / masomo hayangemfaa kitu katika maisha ya ndoa.

( Hoja 4 x 1 = alama 4 )
( 1 ya utiririko )

KUSAHIHISHA

| | | |
|---|---|---|
| Maudhui | (a) 8 | (1) Ondoa makosa 6 ya sarufi alama 3 ( ½ x 6 ) |
| | (b) 4 | (2) Ondoa makosa 6 ya hijai alama 3 ( ½ x 6) |
| Utiririko | 3 | (3) Maneno ya ziada maneno 10 ya mwanzo – 1 |
| | 15 | (4) Maneno 5 = ½ |

3. MATUMIZI YA LUGHA

(a) (i) ’ n + ge √1
’ M + vua
’ ng , + ombe
’ M + bwa
’ M + tu
’ Mu + K + ta + sa + ri ( moja tu )

(ii) -alik - √1

(b) Changarawe iliyokuwa ufuoni imechafuka.

(c ) Kiwakilishi √ ½ ngeli – A. √ ½
Kiwakilishi kirejeshi √ ½ cha ‘O’ – ye. √ ½

(d) Yeye √ ½ yu √ mzima √, hana neno. 4 x ½ = 2

(e) Nikisoma kitabu hiki vizuri nitafuzu. √1

(f) Yule mbaya mno ashtakiwe.
Ile nzuri inastahili mfalme. 1 x 2 = 2

(g) Mgeni aliyefika aliondoka. 1 x 2 = 2
Mgeni ambaye alifika aliondoka.

(h)

| S √ ½ | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| KN √ ½ | | | KT √ ½ | | |
| N √ ½ | V √ ½ | N √ ½ | $T_s$ √ ½ | T √ ½ | E √ ½ |
| dalili | za | ukimwi | zinaweza | kujificha | sana |

10 = 4
9 = 3 ½
8 = 3
7 = 2 ½
6 = 2
5 = 1 ½
4 = 1
3 = ½
(0 – 2) = 0

(i) Liwa, L –iw – a 1 x 2 = 2

(j) Tuliondoka Nairobi mwendo wa saa tatu asubuhi kwa sababu hatukutaka kutatizika njiani, ilibidi tule mapema. Wajua watu husema, " cha mtu ni alo nacho tumboni" .

9 = 3
7 – 8 = 2 ½
6 = 2
5 = 1 ½
4 = 1
2 – 3 = ½
1 = 0

(k) Alisita – mofimu tegemezi .
Sita mofimu huru. 2 x 1 = 2

(l) Hatujachukua √ 1 nguo chache kuuza √1 2 x 1 = 2

(m) - Panya wote wanaotusumbua hapa kwetu nyumbani watauliwa na paka niliymleta.
- Panya wote wanaotusumbua hapa kwetu nyumbani watauawa na paka niliyemleta.
- Panya wote wanaotusumbua hapa nyumbani watauliwa na paka ambaye nimemleta.

(n) Baba ingia ndani!
Baba! Ingia ndani!
Ingia ndani baba! 1 x 2
Baba, ingia ndani!
Baba ingia ! ( * Akiandika ingia ndani! = 1 )

(o) - Jane alikula chakula chote.
- Jane alitumia ufagio kuondoa chakula kilicho. 2 x 1 = 2

(p) Kwa uhodari - Kirai kielezi
√1 √1 = 2

(q) "Nitarudi kesho". Mzazi alisema 1 x 2 = 2

(r ) Nipatie kitabu ambacho nilikupatia.
Nipatie kitabu nilichokupatia. 1 x 1 = 1

4. ISIMU JAMII

(a) Sajili ya darasani katika mazingira ya shule / ofisi shuleni.
Thibitisho : Msamiati kama matokeo ya muhula kuwa duni waonyesha umuhimu mkubwa unaotiliwa matokeo bora ya mitihani kwa upande wa wanafunzi.
‘ Kulingana na vijana wabaya’ yaonyesha umuhimu wa nidhamu katika mazingira ya shule ili matokeo bora yapatikane.

(b) (i) Lugha huwa ni sanifu yenye ufasaha na sahihi kisarufi.
(ii) Sentensi ndefu
Sentensi za mwalimu aghalabu huwa ndefu.

(iii) Huwa na mwazilishi mkuu.
Mara nyingi katika mazingira ya shule kiasi kikubwa cha mawasiliano hutoka kwa mwalimu.

(iv) Misamiati ya taaluma mbalimbali.
Lugha ya darasani huwa na misamiati na istilahi nyingi za kitaaluma kutengemea uwanja wa kitaalam unaoshughulikiwa – lugha, sayansi n.k

(v) Kurejelea mawazo ya wengine
Lugha ya darasani hurejelea mawazo na kazi za watu wengine hasa katika somo la dini, fasihi, historia n.k

(vi) Kuna urasmi Fulani wa lugha.
Lugha ya darasani ina urasmi mwingi. Kuna utaratibu maalum wa nani aseme nini na aseme kwa namna gani. Kawaida mwanafunzi huongea kwa idhini ya mwalimu.

(vii) Lugha yenye heshima na adabu.
Lugha ya darasani huwa na heshima na adabu. Mwanafunzi huonyesha adabu kwa walimu wake, hunyenyekea ili apate usaidizi n.k

(viii) Mbinu maalumu
Lugha ya darasani hutumia mbinu maalumu ambazo husadidia kuelekeza wanafunzi katika kazi zao. Matumizi ya maneno kama vile : kwanza, tena, mwisho kabisa huelekeza aidha zilipo hoja au mwisho wa hoja.

Jina _____ Nambari _____

Sahihi ya mtahiniwa _____

Tarehe _____

**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**FASIHI**
**JULAI / AGOSTI 2011**
**MUDA : 2 ½**

**TATHMINI YA PAMOJA YA WILAYA YA MAKUENI / KATHONZWENI 2011 (MAKA)**
**Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**SAA : 2 ½**

**MAAGIZO**

Jibu maswali manne pekee
Swali la KWANZA NI LA LAZIMA.
Maswali yale mengine matatu yachanguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi and Fasihi Simulizi.
Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

***Kijitabu hiki kina kina kurasa 3 ambazo zimepigwa chapa***

***Fungua ukurasa***

TAMTHILIA
Kithaka wa Mberia: KIFO KISIMANI.
Swali la Lazima.

1,. Ndoto ni mbinu ya kubashiri matukio au hali ya baadaye. Kwa kurejelea ndoto mbili katika Tamthilia “Kifo Kisimani” thibitisha madai haya. (alama 20)

RIWAYA
S.A. Mohamed : UTENGANO
Jibu swali la 2 au la 3

2. “Mwiba wa kujichoma hauna kilio”
Onyesha jinsi methali hii inavyooana na yaliyomo katika Riwaya ya Utengano” (alama 20)

3. “Mara ngapi kakaangu nimekuwaza juu ya mwendo wako? Lakini umejisahau kabisa wewe umetoka wapi / ulikuwa nani? Ulikuwa vipi wakati wa ukoloni? Unalojua sasa ni kulimbika mali”

(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 6 )
(b) Onyesha sifa za wahusika hawa kwa mujibu wa mazungumzo haya. (alama 14)

HADITHI FUPI : MAYAI WAZIRI WA MARADHI
K.W. WAMITILA NA HADITHI NYINGINE.
Jibu swali la nne au la tano.

4. “Akilini alikuwa akiyacheua mafundisho ya leo kanisani, alikwenda kwa ajili ya kukipata chakula cha kiroho.”

(a) Ni nani anayerejelewa ? ( alama 2 )
(b) Eleza kwa kirefu masaibu yaliyompata anayerejelewa. (alama 10)
(c ) Onyesha jinsi kinaya kinavyojitokeza katika hadithi hii. (alama 5 )
(d) Eleza hulka ya anayerejelewa. (alama 3 )

5. (a) Neno kumi limetajwa kwa njia kadhaa katika hadithi ya Mayai Waziri wa Maradhi. Fafanua kwa kutoa mifano halisi. (alama10)
(b) “Uongozi ni swala lililoshughulikiwa sana katika hadithi ya Mayai Waziri wa Maradhi.” Thibitisha. (alama 10)

FASIHI SIMULIZI

6. (a) (i) Nini maana ya ngomezi. ( alama 2 )
(ii) Fafanua sifa tano za ngomezi. ( alama 5 )
(iii) Taja mifano mitatu ya Ngomezi za kisasa. ( alama 3 )
(b) (i) Maghani ni nini? ( alama 2 )
(ii) Eleza fani zifuatazo za maghani.
(a) Vivugo
(b) Tondozi
(c ) Pembezi
(d) Rara ( alama 8 )

USHAIRI

***Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.***

1. Tunda ni kuliangua, chungwa liloninginia,
   Tunda pia kuchumia, mbuga sima yowelea,
   Jinginelo lipo?

2. Tunda kivuno shambani, lima kisha palilia,
   Tunda vinono nyumbani, kwa jasho shughulikia
   Jinginelo lipo?

3. Tunda tokeo la kazi, na ujira jipatia,
   Tunda matokeo wazi, jitihada jifanyia,
   Jinginelo lipo?

4. Tunda pia ni kizazi, wana hao niliozaa,
   Tunda tama ya ulezi, wana wataponifaa,
   Jinginelo lipo?

5. Tunda letu la uhuru, minyororo jikongoa,
   Tunda sote kuwa huru, na mazao furahia,
   Jinginelo lipo?

6. Tunda ni wetu uchumi, na chumo kujichumia,
   Tunda mwenzangu huchumi, ukaweza kwendelea
   Jinginelo lipo?

7. Tunda bora utu mwema, yako roho kuilisha,
   Tunda la roho nasema, mja kumkamilisha,
   Jinginelo lipo?

Maswali

(a) Shairi hili lina babari kadha zitaje na ueleze. ( alama 4 )
(b) Eleza vina na mizani ya ubeti wa sita na saba. (alama 4)
(c ) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (alama 4 )
(d) Taja mbinu ya lugha iliyotumika katika shairi hili. (alama 2 )
(e) Taja maana ya ‘tunda’ kama ilivyotumika katika shairi. (alama 3 )
(f) Eleza maana ya maneno haya kama ilivyotumika katika shairi. (alama 3 )
   (i) Kuliangua
   (ii) Palilia
   (iii) Kujichumia.

**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**FASIHI**
**JULAI / AGOSTI 2011**

**TATHMINI YA PAMOJA YA WILAYA YA MAKUENI / KATHONZWENI 2011 (MAKA)**
**Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

SWALI LA KWANZA (LAZIMA)

Q1. Ndoto ni ruya au maono/mawazo yanayomjia mtu akilini wakati amelala. Mara nyingi ndoto huwa utabiri wa matukio ya baadaye katika kazi ya msanii. Vilevile ndoto huweza kueleweka kama tahadhari kuhusu jambo Fulani. Mlengwa katika ndoto huweza kuzuia matukio iwapo anaweza kurekebisha tabia na mienendo yake. Wazo hili linaadhirika katika ndoto ya kwanza.

(a) (i) Ndoto ya Bokono ambapo aliota kwamba watu walikuwa wakimzika kaburini akiwa hai kwa kumfukia kwa udongo. Kwa mujibu wa mkewe Nyalwe ambaye alimsikia akiwika usingizini. Bokono alifoka kwa ukali akiwaambia waliokuwa wakimzika wamwondoe kaburini na wakome kumfukia udongo. Zaidi ya haya anasema kwamba nia ya wanaomzika ni kuchukua uongozi wake.

(ii) Baada ya Bokono kumfafanulia Nyalwe ndoto yake, mazungumzo marefu yanatokea kati yao. Nyalwe anamkumbusha Bokono kwamba uongozi wake ulikuwa mbaya kwa hivyo asiporekebisha mienendo yake na vibaraka wake kina Batu, angepokonywa uongozi.

Nyalwe anaendelea kumweleza jinsi alivyokuwa akidanganywa na vibaraka wake kwamba uongozi wake ulikuwa mzuri na alipendwa na watu. Ili kudhihirisha uongozi huu mbaya na jinsi vibaraka wake walivyotumia mamlaka vibaya, anamtajia malalamiko ya mama Agoro mkewe Mbino kwamba mgawa ardhi alimpa Askari mkuu uwanja wa kuchezea watoto.

(iii) Ndoto hii inaelezea ukweli wa matukio ya baadaye. Baada ya kifo cha Mwelusi, Umati wa watu ukiongozwa na Azena, Atega, Askari 1 na Kame, unavamia ukumbi wa utawala wa Butangi na kumkamata Bokono na vibaraka wake kina Batu. Atega anasema watahukumiwa na Baraza la Hukumu ambalo lingeundwa upya ili kutowapendelea. Hali hii inaonyesha mapinduzi yaliyotokea Butangi na kumnyang'anya Bokono uongozi kwa nguvu.

(b) (i) Ndoto ya Tanya anayofafanulia Atega na Andua. Katika ndoto hii, Tanya anaota yeye na wenzake wakiwa kisimani walipokwenda kuchota maji. Walipokuwa karibu na kisima, walimkuta simba mkubwa amelala kando ya kisima. Wote waliingiwa na hofu mpaka wakaanza kurudi kinyumenyume ili kutorokea janga lile. Mmoja wao alipochugulia vizuri aligundua kwamba huyo simba alikuwa amekufa.

Tanya anaendelea kusema kwamba ndoto hii ilikuwa ikienda na kurudi. Pia ilikuwa na sura nyingi. Kichwa cha simba mara kilikuwa kinabadilika na kuwa sura ya Mwelusi.

(ii) Ndoto hii ni utabiri wa kifo cha Mwelusi. Mwelusi alipotoroka gerezani, yeye na Atega walielekea kwenye kiisma cha mkomani ambapo ilikuwa marufuku kuchota maji. Zigu alikuwa anakichunga kisima ili yeyote asifanye hivyo. Siku hii Andua dadake Mwelusi pamoja na watu wengine walikuwa pale waking'ang'ania kuchota maji kwa nguvu Wakati Mwelusi na Atega walikuwa wanatetesha Zigu kwa kuwazuia watu kuchota maji, Gege anaingia na kumwambia waende chemba ili ampe ujumbe kutoka kwa mamake. Baada ya Mwelusi kutoroka gerezani, vibaraka wa Bokono, Batu, Mweke na Talui walimshawishi Gege kumwua kakake kwa kuahidiwa kuozwa Alida bintiye Bokono pamoja na zawadi zingine aliposhawishika vya kutosha, alikimbia nyumbani na kuuliza alikokuwa Mwelusi. Mamake alipoahidi kwamba Gege alikuwa na nia ya kuomba msamaha, alimwelekeza pa kumpata. Pale kisimani, alipomwita waende chemba, alimdunga kisu tumboni akamwua.

Mwelusi alikuwa mzalendo katika Butangi ambaye alitegemewa kuleta mapinduzi ya utawala dhalimu. Simba ni mnyama muhimu mwituni kwani huogopwa na wanyama wengine na pengine huwazuia kutoangamizwa na maadui kama vile binadamu. Kifo cha Mwelusi kinalinganishwa na kifo cha simba.

(iii) Sura nyingine yaweza kuwa ya Mtemi Bokono. Yeye alikuwa kiongozi wa Butangi ambaye aling'ang'ania kubaki kama kiongozi hata baada ya utawala wake kuwa mbaya. Kukamatwa kwa Bokono na wafuasi wake baada ya kifo cha Mwelusi, kunaonyesha mapinduzi yaliyofanywa na wanabutangi na kumpokonya uongozi. Yeye kama kiongozi ni mfano wa simba aliyeuawa kwani alikuwa mtu mashuhuri.

Hakiki maelelzo mwafaka ya ndoto hizi mbili
(a) Ndoto ya Bokono = alama 10
(b) Ndoto ya Tanya = alama 10

2. RIWAYA : UTENGANO

- Maksuudi alipomtaliki Tamima alisababisha utengano wa aila yake na kifo cha kitoto kichanga.
- Kwa kushiriki biashara haramu, Maksuudi alijisababishia kifungo cha miaka miwili na kupoteza kazi na hadhi yake.
- Maimuna anashindwa kutambua hila za walimwengu waovu na kujikuta katika shida akiwa pumziko.
- Kwa kuvunja kanuni za wazazi wake za kutawishwa zinampelekea Maimuna kujuta baada ya kupoteza hadhi na kudharaulika, James anataka kumtumia vibaya.
- Farashuu alimharibu Maimuna akidhani amwadhibu Maksuudi. Maimuna anaolewa na Kabi, mjukuu wake.
- Maksuudi anakosa kiti cha ubunge kutokana na uovu wake. Kazija anaonyesha ila za Maksuudi katika mkutano wa uhuru.
- Zanga akosa kuchaguliwa mbunge kutokana na ubinafsi wake wa kulimbikiza mali – magari na nyumba tatu.
- Mussa apigwa na babake kutokana na ufamanizi kwa Kazija – ajihusisha na mwanamke aliyemzidi umri.
- Maksuudi alipomkosea Mwanasururu apaswa kujilaumu kwa kusambaratika kwa familia yake.
- Kipigo cha Maksuudi pale Rumbatola kulisababishwa na yeye mwenyewe kujiingiza jukwaani na kutibua tafrija.
- Aidha apaswa kujilaumu kwa kutomsikiliza Rashid na kujizuia.
- Tamima apaswa kujilaumu kwa kutochukua hatua dhidi ya Maksuudi kama alivyofanya Binti Kocho.
- Yeye alimnyenyekea kupita kiasi Maksuudi akamwadhibu kijeuri. Zozote 10 x 2 = 10

3. (a) Mzungumzaji ni Fadhili akimzungumzia Maksuudi. Hapa ni nyumbani kwa Maksuudi ambapo Fadhili amemtembelea Maksuudi baada ya yeye kumualika kwake nyumbani. Fadhili alipoingia alimkuta nduguye akifanya mazoezi katika tepurekonda jinsi atakavyoshawishi umma kumchagua kama mbunge katika kampeni zilizokuwa zinakaribia. Fadhili alikuwa ameitikia mwito wa ndugu yake ndiposa alifika kwa Maksuudi siku hiyo.

(alama 6)

**Maksuudi**

- Ni mtumishi wa umma na mfanyi biashara.
- Alikuwa maskini aliyetokana na tabaka la wakulima, tabaka la wanyonge.
- Alikuwa mwanaharakati wa kupigania uhuru, na umma ulimzawadi Maksuudi kwa kumpa wadhifa wa Mkuu wa Wilaya, mwenyekiti wa chama na mkurugenzi wa shirika la Bima la Taifa.
- Baada ya kupata vyeo hivi, Maksuudi alibadilika na kuwa mwenye tamaa na ubinafsi mwingi.
- Ndipo alianza kujilimbikizia mali kwa kuhini, kunyang'anya na kwa njia za dhuluma.
- Baada ya kutajirika, Maksuudi alianza kuwatesa waliomnyanyua na hasa aliuelekeza udhalimu wake kwa wanawake.
- Ni tajiri, mtawala asiyewajibika na msaliti.
- Ni mwizi na pia katili
- Ni kielelezo cha upinzani na kuzingiti cha maendeleo ya wanawake.
- Amesaliti Imani, ndoto na matarajio ya waliokuwa nayo wananchi walipopata uhuru.

**Fadhili**

- Ni Inspekta wa Polisi
- Ni mtumishi mwaminifu anayetambua kuwa cheo na wadhifa alionao ni dhamana.
- Anatokana na tabaka la wakulima na wafanyikazi kama nduguye.
- Ni mtetezi wa kweli wa wanyonge.
- Ana msimamo thabiti na nia ya kuendeleza maslahi ya wanyonge walio wengi.
- Anamwasa nduguye dhidi ya mwendo wake mbaya na kumkanya kutotmia mamlaka yake vibaya.
- Ni kiongozi aliyewajibika, anajali na kuweka maslahi ya umma mbele ya yale yake binafsi.
- Ni kielelezo cha viongozi wanaoelewa mianzo na viini vya umaskini katika jamii.,
- Hayuko tayari kuisaliti imani ya umma kutokana na vishawishi vya rushwa na hongo.

( 7 x 1 = 7 )

4. MAYAI WAZIRI WA MARADHI NA HADITHI YINGINE

(a) Anayerejelewa ni Likono ( 2 x 1 )

(b) Masaibu ya Likono

- Kugongwa na gari na kuumia
- Kurukwa na kizito kibambo
- Kizito kibambo kutoroka kabisa bila kulipa pesa alizodaiwa amlipie Likono.
- Watoto wa Likono kufukuzwa shuleni kwa kutolipiwa karo.
- Bintiye Rita kukosa kazi, licha ya Likono kutoa hongo

| | |
|---|---|
| Kutaja masaibu | (alama 1 ) |
| Kueleza | (alama 1 ) |
| Zozote | ( 5 x 2 = 10 ) |

(c ) **Kinaya**

- Anwani ya hadithi msamaria mwema ni kinaya
- Kizito alijiita msamaria mwema na ndiye aliyemgonga Likono.
- Mshahara wa Likono kusimamishwa anapohitaji pesa zaidi.
- Hospitali ya Gipfel kuthamini pesa kuliko utu.
- Daktari wa Gipfel kusisitiza kuwa Likono oparesheni ya dharura lakini alipona bila operesheni yoyote. (alama 5 )

(d) **<u>Hulka ya Likono</u>**

- Anayejali maslahi ya familia yake.
- Asiyekata tamaa – mwenye matumaini ya mambo mazuri.
- Mtulivu – hata kizito anaposema mambo ya uwongo yeye anakuwa mtulivu.
- Mtiifu – anafuata kila jambo bila kupinga.
- Hapendi kulalamika – licha ya maumivu makali hasemi chochote.

( 3 x 1 = 3 )

5. (a)
- Watoto kumi walizaliwa siku ya uhuru.
- Watoto kumi waliokondeleana walimjia Mayai usiku kama mizuka.
- Sherehe iliyoandaliwa ya kusherehekea mwaka kumi na uhuru.
- Ukombozi alienda saa kumi
- Mzee Moris alipiga ngoma kumi katika sherehe.
- Mkombozi alikuwa wa kumi nyuma ya watoto kumi.
- Mfanyikazi wa Mayai aliwaacha watoto wake wakijiandaa kwenda kwenye sherehe ya miaka kumi ya uhuru.
- Mayai Waziri alimpigia simu Balozi wa nyumba kumi.

( 5 x 2 = 10 )

(b)
- Viongozi wana tamaa ya kulikimbiza mali. Mayai na mawaziri wenzake wanapora mali za umma na kuendeleza utabaka.
- Viongozi ni wanafiki. Mayai anahudhuria mkutano wa Rais kisha anatorokea.
- Viongozi wafurahia maafa ya raia. Mayai anafurahia magonjwa maangamizi.
- Viongozi wanaendeleza ukoloni mamboleo: Waishi katika majumba makubwa.
- Viongozi kutowajibika. Daktari pondamali kukataa kumsaidia Mayai alipotaka kujua zaidi juu ya mizuka.
- Viongozi kuwa mafisadi. Mayai anaelezea kuridhika kwake katika kazi ya uwaziri na kukashifu ile ya ualimu kwa sababu hakupora chochote ila kusumbuliwa na waunguzi kwa migomo.
- Viongozi kutotekeleza ahadi zilizotolewa katika makongamano. Hii ndiyo sababu ukombozi wa mizuka wenzake wanatia alama ya X katika majina ya mawaziri wale.
- Sherehe ya miaka kumi baada ua uhuru haina maana kwani hakuna kilichofanyika kwa miaka hiyo yote.

Zozote 5 x 2 = 10

6. FASIHI SIMULIZI

(a) (i) Ngomezi ni fasihi ya ngoma.

(ii) Sifa za ngomezi

- Hufumba ujumbe fulani kwa wasiohusika.
- Hushirikisha zana za muziki zenye mapigo maalum.
- Hutoa matangazo rasmi kuhusu jambo lolote katika jamii husika mf. Kifo, harusi n.k
- Ujumbe wa ngoma hufasiriwa na wanajamii kama inavyokubaliana.
- Hutekeleza majukumu maalum katika jamii.
- Huongozwa na watu katika jamii

( 5 x 1 = 5)

(iii) Ngomezi za kisasa .

(a) Ving'ora.
(b) Kengele (mahakamani, shuleni, kanisani) .
(c ) Milio ya ambulensi, magari ya polisi, mazima moto n.k).
(d) Toni za kengele za simu za rununu.

(b) (i) Maghani ni utungo wa kishairi ambao hutongolewa kwa kutumia sauti iliyo kati ya uimbaji na uzungumzaji. ( alama 2 )

(ii) (a) Vivugo – Maghani ya kujisifu yanayotungwa papo hapo aghalabu na fanani anayejisifu.
(b) Tondozi – Ni utungo wa kutukuza watu, wanyama, vitu nk. Husifu maumbile, sura, tabia na matendo.
(c ) Pembezi - Husifu watu wa aina fulani katika jamii kutokana na mchango wao tu matendo yao mf. Viongozi, wanamichezo, wanamuziki n.k.
(d) Rara – utungo wa kishairi ambao husimulia mambo ya kubuni. Hutongolewa na kughaniwa kwa kusudi la kusisimua hadhira.

7. USHAIRI

(a) Tathlitha – Mishororo mitatu kila ubeti
Kikwamba – neno tunda kurudiwa rudiwa
Msuko – Kibwagizo mizani chache.
Ukara – Vina vya nje vyatiririko – vya ndani vyabadhuabadilika. ( alama 4 )

(b) Vina : Ubeti 6 Ubeti 7.
mi, a ma – sha
mi, a ma, sha
po po

Mizani : ubeti 6 Ubeti 7
8, 8 8, 8
8, 8 8, 8
6 8 ( alama 4 )

(c ) Tunda ni kivuno kinachotoka shambnai baada ya kulima na kupalilia. Mazao mazuri hupatikana baada ya kushughulika kwa jasho. Je, kuna lingine? ( alama 4 )

(d) Balagha (alama 2 )

(e) - Zao la mti
- Tokeo la kazi
- Kizazi / watoto
- Uhuru
- Uchumi
- Vitu wema
- Kutoa matini

(f) (i) Kutunda
(ii) Kulimia
(iii) Kujitafutia riziki ( alama 3 )